



Kinga rahisi ya ugonjwa wa figo kwa kuwalenga waliyoko hatarini kuathirika

Siku ya Figo Ulimwenguni 2020: Kila mtu kila mahali kinga ni bora kuliko kutibu

Mtu mmoja kati ya watatu ulimwenguni yumo hatarini kuathirika na maradhi sugu ya figo (MSF). Hali kadhalika, asilimia 10 ya watu wote ulimwenguni wana maradhi sugu ya figo na takwimu zasema takriban watu 9 kati ya 10 wenye maradha hayo hawajuwi kwamba wana ugonjwa huwo.

Kutokana na hali hii, katika Siku ya Figo Ulimwenguni (SFU) ya mwaka huu, itakayoadhimishwa Alhamisi tarehe 12 Machi, Jumuiya ya Kimataifa ya Taaluma ya Figo (ISN) na Shirikisho la Kimataifa la Nyakfu za Figo (IFKF) watahindikiza umuhimu na ulazima wa kuwaelimisha umma, wagonjwa, madaktari, na waundaji sera juu ya hatua za kujikinga na ugonjwa wa figo.

Kauli mbiyu ya maadhimisho ya mwaka huu inayosema “Afya ya Figo kwa kila mtu kila mahali – kuanzia kinga, ugunduzi hadi kuaguliwa” inatiliya mkazo umuhimu wa hatua za kinga – ugonjwa unapoanza, unapokua na unapoanza kuwa sugu hadi kufikia dondandugu.

Asilimia 2 hadi 3 ya bajeti ya afya ya nchi zilizoendelea hutumiwa kwa kusafisha na kutiwa figo mpya kwa watu wachache sana wa nchi hizi. Gharama ambazo zaepukika kwa kukinga uharibifu wa figo. Fauka ya hayo, gharama inaweza kushuka zaidi au kupunguzwa nusu kwa nusu lau hatua za kinga zitachukuliwa na kuangaliwa vizuri waliyo hatarini kuathirika kama wenye kisukari kikali, presha na wanaodhoofika haraka kwa MSF.

Profesa Philip Kam-Tao Li wa Hospitali ya Prince of Wales katika Chinese University of Hong Kong, Hong Kong anasema, “Kinga za kimsingi zilenge kubadili hatari za MSF na kushughulikia usokawaida wa figo na njia ya mkojo, na hatari zitokanazo na mazingira na sumu ndani ya figo”. Naye Profesa Guillermo Garcia wa University of Guadalajara Health Sciences Center, Mexico amefafanua zaidi kwamba, “Kinga za upili zinazojumuisha kuuchunga mshindikizo wa damu, kudhibiti sukari na kuwacha chakula chenye protini na sodiam nyingi liwe ndilo lengo la hatua za kielimu na kimatibabu kwa watu wanaoanza ugonjwa wa figo”. Anaongezea kuwa, “Kwa wagonjwa wenye MSF, wastani hadi juu, uangalizi wa magonjwa ya damu chafu na moyo na ulaji wa chakula chenye protini kidogo ndizo hatua zinazopendekezwa ili kuepuka au kuchelewesha kupachikwa figo mpya.

Profesa Li, aliyekuwa Rais wa Jumuiya ya Taaluma ya Figo ya Asia Pacific anasema, “Juhudi za kitaalimu na kisiyasa zahitajika ili kueneza **fikra ya kinga**. Haswa, kunahitajika, kutokana na kampeni za kimataifa, kuwafanya watu wajuwe hatari zilizopo na kuwashajiisha wagonjwa kwa kuwapa nafasi za kimtandao kujifunza. Madaktari nao watafaidika kutokana na mafunzo mahsusi na kuweza kuwatambuwa wagonjwa waliyoko hatarini na wanasiyasa hawana budi kuikubali na kupa umbele miradi hii. Miradi ambayo ina gharama ndogo lakini athari kubwa kwa mfano: kuwachunguza watu waliyoko hatarini mwa MSF, kupatikana kwa wepesi matibabu ya MSF, kupatikana kiurahisi teknolojia za kimsingi na madawa muhimu, na kubadilishana majukumu

baina ya madaktari na wauguzi wa mstari wa mbele katika kusimamia maendeleo ya MSF na njiya nyengine za kinga.

Wafadhili wa Kimataifa wa SFU:

Shukurani kuu ziwaendee wafadhili wetu wa kimataifa waliyowezesha sherehe hii kufanyika ulimwenguni kote. Asanteni sana.



Kuhusu SFU:

Maelezo zaidi kuhusu Siku ya Figo Ulimwenguni tembelea: <https://www.worldkidneyday.org/>

Kuhusu waandaaji wa SFU:

Siku ya Figo Ulimwenguni ni juhudi za pamoja za Jumuiya ya Kimataifa ya Taaluma ya Figo (ISN) na Shirikisho la Kimataifa la Nyakfu za Figo (IFKF).

Jumuiya ya Kimataifa ya Taaluma ya Figo (ISN) iliyoasisiwa 1960, ni shirika la kiulimwengu lisilo la kibiashara lililojikita katika kusaidiwa uangalizi wa figo na kupunguza matukiyo na athari za ugonjwa wa figo ulimwenguni. Miradi ya ISN huleta pamoja juhudi za nchi zilizoendelea na zinazoendelea ili kupambana na kutibu ugonjwa wa figo kimataifa. Kwa maelezo zaidi juu ya ISN tembelea www.theisn.org.

Shirikisho la Kimataifa la Nyakfu za Figo (IFKF) ni shirikisho lisilo la kibiashara lililoasisiwa 1999 na lina nyakfu za figo 63 na makundi ya wagonjwa katika nchi 41. IFKF hushindikiza ulimwenguni kote ubora wa afya, ubora wa hali ya wagonjwa wa figo; husambaza kote viwango bora vya kutibu na kuuguza; husaidiwa kuanzisha nyakfu za figo kule ambako hazipo; na huendeleza utafiti juu ya ugonjwa wa figo. Kwa maelezo zaidi tembelea www.ifkf.org.

Anwani ya mhusika wa tangazo:

Anne Hradsky, Meneja wa kampeni , aliyeko International Society of Nephrology, Brussels, Belgium. T) +32 2 808 04 20 E) anne@worldkidneyday.org

Warejelewa:

Professor Philip Kam Tao Li, Mwenyekiti mwenza wa Kamati ya SFU ya ISN, Prince of Wales Hospital, Chinese University of Hong Kong, Hong Kong. T) + 852 35053616 E) philipli@cuhk.edu.hk

Professor Guillermo Garcia, Mwenyekiti mwenza wa Kamati ya SFU ya IFKF, aliyeko University of Guadalajara Health Sciences Center, Mexico T) +52 1 33 3662 2288 E) ggarcia1952@gmail.com